# DAWASA YETU

TOLEO NO: 207 | TAREHE: 30.6.2025 HADI 6.7.2025

# CHALAMILA ATAKA HUDUMA BORA ZA MAJI KWA WANANCHI



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam **Mhe. Albert Chalamila** ametoa wito kwa Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA**) kuzingatia nidhamu mahali pa kazi na kuwa na ushirikiano kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi wote wa Dar es Salaam.

**Mhe. Chalamila** ameyasema hayo wakati wa kikao cha Watumishi wa **DAWASA** cha kufunga mwaka **2024/25** na kufungua mwaka mpya wa fedha **2025/26** kilicholenga kutoa tathmini ya utendaji kazi kwa mwaka uliopita na kuweka bayana ya mikakati mipya kwa mwaka mpya wa fedha.

"Watumishi mnatakiwa kuwa na umiliki wa kazi yenu ya kutoa huduma kwa wananchi, kwa kufanya kazi kwa kuipenda ili kuleta tija kwa Taasisi na kuwezesha huduma ya majisafi iwe endelevu kwa wananchi kwa muda wote," amesema **Mhe Chalamila**.



Kwa upande wa Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu **DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire** amewapongeza Watumishi kuwa utendaji wa kazi katika mwaka wa fedha uliopita na kuwataka kuongeza bidii zaidi ya kazi katika kuboresha utoaji wa huduma ili kukamilisha malengo yaliyopo.

Amesema kuwa **yapo mafanikio yaliyopatikana ikiwemo ya kuongeza idadi ya wateja kupitia zoezi la maunganisho mapya ya maji yaliyofanyika kwa mwaka wa fedha uliopita**.

**"Kazi kubwa inatakiwa kufanyika kwa mwaka huu ikiwemo kuongeza nguvu katika kuzuia upotevu wa majisafi kwenye maeneo yote ya kihuduma ili kuokoa fedha zinazowekezwa kwenye usambazaji wa majisafi"**.

**DAWASA MOJA, NGUVU MOJA, TUNASONGA MBELE**